

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE

Simu: 028-2227148  
Fax: 028-2227140  
E-Mail ded.karagwe@kagera.go.tz  
ded@karagwedc.go.tz

S.L.P. 20  
KARAGWE



TANGAZO LA ZABUNI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADUKA, VYOO NA BUCHA SOKO LA KAYANGA KWA NJIA YA UBIA 'PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP' (PPP)

22.6.2017

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe anawatangazia wananchi, mtu binafsi, wafanyabiashara, Makampuni au Taasisi yoyote kuwa anahitaji kupata Watu binafisi, Wafanyabiashara, Makampuni au Taasisi atakaingia ubia na Halmashauri Kujenga Vyumba vya maduka, Vyoo na Bucha soko la Kayanga kwa njia ya 'Public Private Partnership' (PPP). Ujenzi wa soko umetengwa katika makundi maalum (Block A,B,C,D na G). Ambapo atakayeshinda zabuni atasaini mkataba na Halmashauri na kuanza kulipia kiasi kama sehemu ya gharama ya ujenzi mpaka atakapo rejesha gharama yote aliyoitumia katika ujenzi wa vyumba vya maduka/ vyoo/ bucha kama ivyoelezwa kwenye nyaraka za zabuni.

NA	AINA YA ZABUNI	AINA	IDADI	NAMBA YA ZABUNI
1	BLOCK A	MADUKA	46	LGA.033/W/PPP/2016/2017/01(LOT 1)
2	BLOCK B	MADUKA	17	LGA.033/W/PPP/2016/2017/01(LOT 2)
3	BLOCK C	MADUKA	28	LGA.033/W/PPP/2016/2017/01(LOT 3)
4	BLOCK D	MABUCHA	12	LGA.033/W/PPP/2016/2017/01(LOT 4)
5	BLOCK E	MADUKA MAKUBWA	8	LGA.033/W/PPP/2016/2017/01(LOT 5)
6	BLOCK G	VYOO	8	LGA.033/W/PPP/2016/2017/01(LOT 6)

**MASHARTI:**

1. Kila mwombaji ni lazima awe ni raia wa Tanzania.
2. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya zabuni ya shilingi 50,000/= kwa kila loti (Block) na kupewa stakabadhi pamoja na kabasha la zabuni ambalo utatakiwa kulijaza na kulirudisha kabla ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ada ya maombi hairudishwi.
3. Mwombaji ambae ni Kampuni aambatanishe nyaraka zifuatazo:
  - i. Nakala ya TIN na VAT
  - ii. Nakala ya leseni ya biashara husika.
  - iii. Nakala ya usajili wa kampuni.
  - iv. Nakala ya stakabadhi ya ada ya maombi.
  - v. Mamlaka ya kisheria ya kusaini mikataba kwa niaba ya kampuni (Power of attorney)
4. Kila ombi litatakiwa kuwa na nakala halisi (Original copy) pamoja na nakakala moja (One copy of the original copy).
5. Ujenzi utazingatia viwango, michoro, muda na taratibu zilizobainishwa kwenye nyaraka ya zabuni.
6. Kikao cha awali kabla ya maombi ya zabuni kuonesha Maeneo ya Ujenzi, na kujibu maswali yote ya ufahamu kabla ya maombi kitafanyika tarehe 28.6.2017 saa 3 asubuhi katika eneo la soko Kayanga.
7. Kila mwombaji atapokea maelezo pamoja na taarifa kutokana na nyaraka za zabuni atakazopewa na Katibu wa Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya Karagwe wa S.L.P. 20, Karagwe, aliyepo kwenye jengo la Halmashauri ya Wilaya Karagwe mjini Kayanga Karibu na Kituo cha polisi Karagwe kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 Alasili Jumatatu hadi Ijumaa ukiondoa siku za mapumziko na Sikukuu
8. Mwombaji zabuni mwenye nia atapatiwa nyaraka ya Zabuni kwa malipo ya shilingi elfu hamsini tu (Tsh. 50,000/=) kwa kulipia benki.
9. Maombi ambayo hayatazingatia masharti yaliyotajwa hayatafanyiwa kazi.
10. Waombaji wote mnakaribishwa kufika wenye au kutuma wawakilishi wenu siku ya ufunguzi. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Katibu wa bodi ya zabuni (W) Karagwe.
11. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 13.7.2017 saa 4.30 asubuhi siku ya Alhamisi na zabuni zitafunguliwa baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe.

Adeodata Augustine

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE

Nakala: Mbao zote za Matangazo  
www.karagwedc.go.tz  
www.ppra.go.tz

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KARAGWE